Nuru ya Kiswahili, Juzuu 1(1), Juni 2022: 119 - 137

# *Utenzi wa Mwana Kupona*: Kilingo cha Utwezaji wa Mwanamume?

**Stella Faustine**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dodoma**

stelafau@gmail.com

**Ikisiri**

*Utenzi wa Mwana Kupona* umevuta nadhari kubwa kwa wasomaji na wahakiki wengi wa kazi za fasihi. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu utenzi huo kwa kukitwa katika mitazamo mikuu mitatu. Mtazamo wa kwanza, unaouona utenzi huo kuwa unamdhalilisha mwanamke; wa pili unautazama kuwa ni utenzi unaosawiri maisha halisi ya mwanamke wa pwani. Mtazamo wa tatu unautazama kama ni kielelezo cha kumdhalilisha mwanamume. Pamoja na tafiti hizo kuweka misingi katika kuuelewa utenzi huo, mtazamo wa tatu unatoa chachu kwa mtafiti kuchunguza kwa kina ni kwa namna gani utenzi huo unamtweza mwanamume. Hii inatokana na kwanza; msukumo unaotolewa na Mbele (1985) ambaye kupitia utenzi huo, anabainisha kuwa kazi ya fasihi ina mawanda mapana ya kiuhakiki na, hivyo, kuwaasa wasomaji wasiwe na mtazamo funge pindi wanapohakiki kazi hizo. Pili, mjadala anaouzua Mulokozi (1999) kwa kuuliza kama utenzi huo unamdhalilisha mwanamke au mwanamume. Tatu, mijadala iliyofanywa kuhusiana na mtazamo wa namna utenzi huo unavyomdhalilisha mwanaume kwa mfano ule wa Mbele (1985) umegusia suala hilo kwa jumla pasipo kufafanua kwa kina vipengele vinavyomdhalilisha mwanamume katika utenzi huo. Uandishi wa makala umezingatia mkabala wa kitaamuli. Data za msingi zilikusanywa maktabani kutoka katika kitabu cha *Tenzi Tatu za Kale* na uwandani. Kwa kutumia misingi ya nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, makala imethibitisha hoja ya msingi kuwa, *Utenzi wa Mwana Kupona* ni kilingo cha kumtweza mwanamume. Hii inatokana na namna mwandishi anavyomjenga mwanamke kwa kumfanya kuwa kiongozi, msaada na nguzo msingi katika maamuzi ayafanyayo mwanamume.

**Dhana za Msingi:** Kilingo, utwezaji, mwanaume, Mwana Kupona

## Utangulizi

*Utenzi wa Mwana Kupona* ulitungwa na Mwana Kupona binti Mshamu katika karne ya kumi na tisa. Mwana Kupona alitunga utenzi huu kama sehemu ya mawaidha kutoka kwa mama kwenda kwa bintiye aliyeitwa Mwana Hashima binti Mataka (Mulokozi, 1999). Lengo ni kumuasa kuhusu masuala mbalimbali ya maisha. Miongoni mwayo ni yale yanayohusu dini, ambapo mtunzi anamtaka binti yake kumwabudu Mwenyezi Mungu kwa kujifungamanisha na dini yake. Anasisitiza pia kuhusu kuishi vyema na mumewe kwa kufuata misingi ya ndoa ili kuleta maelewano na vilevile, kujenga mahusiano mazuri katika jamii.

Kezilahabi (1983) anasema kuwa *Utenzi wa Mwana Kupona* ni utungo pekee wa zamani uliotungwa na mwanamke na kuacha athari kubwa katika maisha ya ndoa Pwani ya Kaskazini. Hii imethibitishwa pia na Mulokozi (1999) anayesema kuwa jamii ya wanawake wa Pwani iliitikia vyema maudhui yaliyomo ndani ya utenzi huo na kuugeuza kuwa ni badala ya asasi ya kale ya unyago iliyokuwa inaanza kutoweka. Wanawake wengi Pwani ya Kenya walinakili na kukariri utungo huo na kuutumia kama sehemu ya malezi kwa kutoa mafunzo kwa mabinti wanaotarajiwa kuolewa.

Kutokana na maudhui yake kugusa suala la mahusiano ya kijinsia kwa jamii nyingi za Waafrika, *Utenzi wa Mwana Kupona* umeibua mjadala mkubwa kwa watafiti na wahakiki wengi wa kazi za fasihi. Kama anavyoeleza Mulokozi (1999), watafiti hao wameutazama utenzi huo katika mitazamo mikuu mitatu. Mtazamo wa kwanza ni ule unaouangalia utenzi huo katika uhasi kuwa unamtweza mwanamke. Miongoni mwa wataalamu wanaojikita katika mtazamo huu ni Mulokozi (1982), Khatib (1985), Mwachofi (1987), Senkoro (1988) na Momanyi (2007). Katika dhana ya kumtweza

mwanamke, watafiti hawa wanafafanua kuwa utenzi huu unamsawiri mwanamke kama kiumbe duni, asiye na thamani na kitu cha kuchezea ili kukidhi uchu wa mwanamume. Khatib (1985) anabainisha kuwa utenzi huo ni sumu mbaya inayorejesha maendeleo nyuma kwani inamweka mwanamke utumwani kwa kumtenga na shughuli za kiuchumi. Mwana Kupona anamjenga mwanamke kama kiumbe dhaifu anayetumikishwa katika shughuli za nyumbani. Miongoni mwa shughuli hizo ni kufua, kupika na malezi ya familia. Mwachofi (1987) anasisitiza udhalilishaji huo kwa kusema kuwa, ili mwanamke aweze kujikomboa, hatakiwi kuyaishi mafunzo yaliyoko ndani ya *Utenzi wa Mwana Kupona*. Hii inatokana na sababu kuwa mafunzo hayo hayajakukusudiwa kumkomboa mwanamke, bali kumweka utumwani kutokana na maudhui yake kufumbatwa na itikadi za mfumo dume.

Mtazamo wa pili unauona utenzi huu kama ni kielelezo cha maisha ya jamii ya Waafrika. Hapa mwanamke anaoneshwa kama kiumbe mwenye wajibu na majukumu makubwa katika malezi ya familia. Miongoni mwa watafiti wanaojiegemeza katika mtazamo huu ni Farsy (1967), Njozi (1990), Gibbe (1993), Sawe (2018), na Mwinyi (2020a) kwa kuwataja baadhi. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa utenzi huo ni mwongozo wa mafunzo anayoyatoa mama kwa mwanawe. Wanafafanua zaidi pale wanapoeleza kuwa *Utenzi wa Mwana Kupona* unaonesha misingi ambayo mwanamke, na hasa wa pwani, anatakiwa kuiishi katika jamii, hususani katika mahusiano ya ndoa. Sengo na Kiango (1974) na El-Maawy (2011) wanafafanua zaidi kuwa utenzi huo ni kibainishi cha majukumu mazito katika malezi ya familia aliyo nayo mwanamke katika jamii. Katika muktadha huu, Sengo na Kiango

(1974) wanabainisha kuwa Mwana Kupona ni mama anayejua wajibu na majukumu yake katika malezi.

Mtazamo wa tatu, unakinzana na mitazamo miwili iliyotangulia. Kama anavyofafanua Mulokozi (1999), madai ya wataalamu wanaojikita katika mtazamo huu ni kuwa wanaompinga Mwana Kupona hawakuelewa undani wa maudhui yaliyotolewa katika utenzi huo. Mbele (1985) anaeleza kuwa yamkini utenzi huo ulitumia kejeli kumwonesha mwanamume kama kiumbe dhaifu anayependa kusifiwa na kurubuniwa na mwanamke kwa vitu vidogo. Pamoja na ufafanuzi anaoutoa, Mbele (1985) anazidi kutueleza kuwa makala yake haikukusudia kuonesha namna mwanamume anavyodhalilishwa kama hitimisho la uchambuzi wake. Lengo kuu lilikuwa kutoa maoni ya jumla kuwa kazi ya fasihi ina mawanda mapana ya kiuhakiki. Msomaji anaweza kuisoma mara nyingi na akaja na maana tofautitofauti kutegemeana na suala la kiwakati, nadharia aliyotumia na muktadha wa upokezi.  Mbele (2014) anafafanua hili zaidi kwa kusema:

> Kazi ya fasihi ikishaandikwa na kuwafikia wasomaji, inakuwa na tabia ya kuleta tafsiri mbalimbali kwa msomaji… Hii inategemea uwezo na uzoefu wake katika kusoma fasihi, akili, imani, itikadi na utamaduni wa jamii. Kwa maana hiyo, *Utenzi wa Mwana Kupona* unaweza kueleweka kwa namna mbalimbali na watu au jamii zenye tamaduni tofauti, na katika vipindi mbalimbali vya kihistoria… Somo la fasihi linatupa fursa ya kuzama katika tafakari, kuchemsha bongo, na hata kuchanganyikiwa. Kuchanganyikiwa ni matokeo ya kufikiri kwa dhati, na ni jambo jema kuliko kukaa tukiwa tumeridhika kwamba masuala ni wazi na rahisi, na kwamba majibu tunayo …

Mitazamo ya watafiti hawa, kama ilivyojadiliwa hapo awali pamoja na mjadala anaouzua Mulokozi (1999) kuhusu kutazama kama *Utenzi wa Mwana Kupona* unamdhalilisha mwanamume au mwanamke,  ndio uliotoa

msukumo kwa mtafiti kuchunguza kwa mapana ni kwa namna gani utenzi huu unamtweza mwanamume kwa kuhusisha maudhui yanayowasilishwa ndani yake na mwitiko wa wasomaji wa kazi ya fasihi.

Katika muktadha huu, makala itaangalia namna *Utenzi wa Mwana Kupona* unavyomtweza mwanamume kupitia mtazamo kuhusu mahusiano ya kimapenzi baina ya mume na mke, mgawanyo wa majukumu katika malezi ya familia, nafasi ya kutoa maamuzi, na pia mtazamo kuhusu thamani ya mtu na utu baina ya mwanamke na mwanamume.

**Kiunzi cha Nadharia**

Utafiti uliozalisha makala hii uliongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Nadharia hii huangazia dhima au majukumu ya msomaji au mhakiki katika matini au kazi ya fasihi (Wamitila, 2002). Wananadharia wenye mwegamo wa mtazamo huu wanajikita katika kuangalia jinsi msomaji anavyoitikia au kuathiriwa na kazi ya fasihi. Mtazamo huu unaakisiwa na kauli inayotolewa na Margaret Atwood kama anavyonukuliwa na Wamitila (2002) kuwa usomaji ni mfanyiko unaombadilisha mtu. Hii ina maana kuwa, unaposoma kazi ya fasihi, huwezi kuwa mtu yuleyule uliyekuwa kabla ya kuisoma. Misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti uliozalisha makala hii ni miwili. Kwanza ni kuwapo kwa vipengele mbalimbali ambavyo huunda mwitikio wa msomaji. Kipengele cha kwanza ni miktadha ya kimazingira na kitamaduni. Katika makala hii vipengele hivi vimezingatiwa katika uchambuzi na uwasilishwaji wa data kwa kuhusianisha mitazamo ya kimazingira mahususi katika jamii za Kiafrika, utamaduni wao na maudhui yanayojitokeza ndani ya *Utenzi wa Mwana Kupona*. Msingi wa pili ni utofauti uliopo kati ya ubaki (uasili) wa umatini husika na hisia binafsi za msomaji. Msingi huu umemwezesha

mtafiti kupanua mawanda ya kiuhakiki kwa kutoa uhuru kwa watafitiwa kutoa mitazamo yao binafsi kuhusiana na *Utenzi wa Mwana Kupona*. Ni katika mtazamo huu ambapo mtafiti na watafitiwa waliweza kuitazama kazi hii kama matini inayoweza kuibua maana mbalimbali kutokana na namna maudhui yake yanavyomwathiri msomaji.

## Methodolojia

Usanifu wa utafiti huu ulikuwa wa kifani. Matokeo ya utafiti yalitokana na uchunguzwaji wa maudhui ndani ya *Utenzi wa Mwana Kupona* kama kiwakilishi cha hali halisi ya maisha ya jamii ya Waafrika kwa kuyahusisha na mwitiko wa wasomaji wa utenzi huo. Mkabala uliotumika katika uchambuzi na uwasilishaji wa data ulikuwa wa kitaamuli. Kama anavyoeleza Ponera (2019), mkabala huu hutumia tafakuri binafsi kwa kuzihusianisha na taarifa mbalimbali za kitafiti, nadharia husika pamoja na ithibati ya data zilizopatikana uwandani na maktabani na kuziwasilisha kwa njia ya maelezo. Sampuli iliyotumika ilikuwa lengwa ambayo ilizingatia sifa za watafitiwa wenye uelewa kuhusu maisha ya jamii ya Waafrika katika muktadha wa utamaduni na wenye ufahamu kuhusu *Utenzi wa Mwana Kupona*. Vitafitiwa vilivyokusudiwa vilikuwa vile vyenye maudhui yanayolandana na mada husika. Kwa kuzingatia miongozo ya utafiti wa kitaamuli na malengo ya utafiti, sampuli iliundwa na makundi yafuatayo: Kwanza ni *Utenzi wa Mwana Kupona*. Pili ni wanafunzi wa Shahada ya Umahiri na Uzamivu (5) kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Tatu ni wataalamu na watafiti wa fasihi ya Kiswahili (4) waliowahi kusoma au kuuhakiki *Utenzi wa Mwana Kupona*. Watafitiwa hawa walikusudiwa kutoa data zinazohusiana na mtazamo wao kuhusiana na maudhui yaliyomo ndani ya *Utenzi wa Mwana Kupona* kwa kuyahusianisha na maisha halisi ya jamii

ya Waafrika. Idadi ya watafitiwa ilizingatia aina ya utafiti, mawanda pamoja na utoshelevu wa data.

**Matokeo ya Utafiti**

Sehemu hii inajadili mawanda ya mtazamo wa wahakiki wanaobainisha kuwa *Utenzi wa Mwana Kupona* unamdhalilisha mwanamume kwa kuhusianisha maudhui yanayopatikana ndani ya utenzi huo na mwitiko wa wasomaji wa kazi za fasihi. Makala inabainisha hili kupitia masuala mbalimbali yanayodhihirisha suala la mahusiano ya kijinsia katika jamii. Masuala hayo yanajadiliwa katika vipengele vinavyofuata vya makala hii:

**Mahusiano ya kimapenzi katika ndoa**

Mahusiano katika mapenzi ni jambo ambalo linakitwa katika ushiriki wa pande mbili. Hii inamaanisha kuwa wote, mwanamume na mwanamke, wana wajibu sawa katika utekelezaji wa tendo hilo (Mwinyi, 2020a). Katika *Utenzi wa Mwana Kupona*, suala hili limetazamwa kinyume na mtazamo huo, ambapo linasisitizwa kama jukumu la msingi la mwanamke na kwamba mwanamume ni mnufaikaji wa jukumu linalotimizwa na mwanamke. Jambo hili linathibitishwa na namna Mwana Kupona anavyomsisitizia binti yake kuwa ndiye anapaswa kuwa mwajibikaji mkuu katika mahusiano ya ndoa ili kumridhisha mwanamume. Katika ubeti wa 31, anasema:

> Kilala siikukuse
> mwegemee umpapase
> na upepo asikose
> mtu wa kumpepea (Mulokozi, 1999:128)

Katika ubeti huu, Mwana Kupona anamsisitizia binti yake kutimiza majukumu yake ya ndoa kwa kuhakikisha anamridhisha mumewe kwa kumpapasa na kumpepea. Kimsingi, majukumu ambayo Mwana Kupona

anamuhimiza binti yake kuyatekeleza ndiyo yanayowafanya baadhi ya watafiti kama Mwachofi (1987) kumlaumu Mwana Kupona kwa kumweka mwanamke utumwani pale anapoliweka jukumu la mapenzi katika upande mmoja. Hata hivyo, Aginiwe Sanga (2020)[1] katika mahojiano uwandani anafafanua kuwa Mwana Kupona kumbebesha binti yake jukumu la kuyaendesha mapenzi katika mahusiano baina ya mume na mke si kwamba anamdhalilisha. Anafafanua kuwa jukumu hili linaonesha nafasi ya mwanamke kuwa ni mtu anayeweza kutimiza jukumu hilo na mwanamume ni mtu wa kusubiri kufanyiwa kwa sababu hana uwezo binafsi wa kufanya hivyo. Anaeleza haya kwa kusema:

> Tunapojadili maudhui ya *Utenzi wa Mwana Kupona* kwa kuyafungamanisha na miktadha ya kitamaduni, mara zote, tunaifinya kazi ya fasihi kujipambanua katika mawanda mapana ya kiuelewa. Hii inasababisha, mara zote, kujifungamanisha katika uelewa uleule wa mifumo jadi kuwa mwanamke anatakiwa awe vipi. Ukishakuwa na mtazamo wako kichwani ambao umekwishaufunga mahala, basi huwezi ukatoka huko wala kuzalisha mtazamo mpya. Kwa mtazamo wangu, hapa Mwana Kupona hajamweka mwanamke katika utumwa wa mapenzi kuwa ni mtu wa kutumika bali amemdhalilisha mwanamume kama kiumbe dhaifu asiyejiweza na mwanamke ndiye dereva.

Hoja ya mtafitiwa huyu inazua maswali kama je, kinachoongoza au kupelekea tendo fulani kufanyika katika ustadi au uzuri ni dhaifu au ni imara? Katika kujibu swali hili, ni wazi kuwa siku zote imara ndiyo inayoongoza. Mtazamo huu unatufanya kubaini kuwa mawaidha anayoyatoa Mwana Kupona kwa binti yake ni kibainishi cha udhaifu wa

[1] Aginiwe Sanga ni mhadhiri ambaye ni mtaalamu wa Fasihi ya Kiswahili, Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano yalifanyika tarehe 12/04/2020 mkoani Dodoma.

mwanamume katika suala la mapenzi kwani hutegemea ustadi wa mwanamke katika ukamilifu wa tendo zima.

**Mgawanyo wa majukumu katika malezi ya familia**

Mgawanyo wa majukumu katika familia ni kipengele kingine kinachobainisha udhaifu wa mwanamume katika kutekeleza masuala mbalimbali kwa jamii. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona*, mtunzi anaonesha kuwa na imani na mwanamke katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya kifamilia. Mwana Kupona kumuusia mwanawe, ambaye ni mwanamke, kuihudumia familia katika masuala mbalimbali kama vile chakula na kuleta umoja na mshikamano, ni kiashiria tosha kuwa, ili familia iweze kuwa imara, ni lazima mwanamke atekeleze majukumu yake ipasavyo. Katika ukinzani wa kimaudhui, baadhi ya watafiti kama vile Mwachofi (1987) na Senkoro (1988) wanayaona majukumu ambayo Mwana Kupona anamkabidhi binti yake kama ni kifungo kinachomweka mwanamke utumwani. Hata hivyo, pamoja na ukinzani huo makala hii imebaini kuwa wosia huu unabainisha wazi kuwa nguvu ya mwanamke katika malezi ni kubwa kuliko aliyonayo mwanamume. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa Mwana Kupona, mwanamume ni kiumbe dhaifu anayetakiwa kulelewa na kuongozwa katika misingi sahihi anayoijenga mwanamke ndani ya familia. Katika kuonesha umuhimu wa mwanamke katika utekelezaji wa majukumu ya familia, Mwana Kupona anamsisitizia binti yake kumhudumia mume ipasavyo pale anaposema katika ubeti wa 33 na 35, mtawalia:

Chamka Simuhuli
mwandikie maakuli
na kumtunda muili
kumsinga na kumwoa

> Mtunde kama kijana
> asiyojua kunena
> kitu changalie sana
> kitokacho cha kungia (Mulokozi, 1999:128)

Nukuu hizi zinaonesha majukumu aliyonayo mwanamke katika malezi ya familia. Kwanza katika ubeti wa 33, Mwana Kupona anamuasa binti yake kumhudumia mumewe kwa kumpa chakula. Pia, anamuasa amlee kama kijana ambaye bado hajui hata kuongea (taz. ubeti wa 35). Malezi haya ambayo mwanamke anaelekezwa kumpa mwanamume yanaonesha wazi nafasi ya mwanamume katika jamii kuwa ni kiumbe dhaifu ambaye, hata katika umri mkubwa, bado anategemea malezi ya mwanamke. Akifafanua hili, Martina Duwe (2020)[2], anasema:

> Mwana Kupona anamtazama mwanamume kama mtoto mdogo. Mzani wa mahusiano ya mwanamume na mwanamke katika malezi ya familia hauko sawa. Ukiangalia katika kazi yake, mwanamke ndiye amepewa majukumu mazito ya kuhakikisha kuwa familia inaenenda katika misingi bora. Hii ni pamoja na kuangalia huduma za mwanamume. Ukijiuliza ni sababu zipi Mwana Kupona anamsisitizia mwanamke kumhudumia mwanamume, utapata jibu kuwa ni kwa sababu mwanamke anaweza. Na kama mwanamke anaweza mpaka kumhudumia mwanamume, ina maana mwanamume ni kiumbe asiyejiweza.

Nafasi ya mke katika kumlea mwanamume imefafanuliwa pia na Marryam Mwinyi (2020b)[3]. Akijikita katika mtazamo jadi ambao unaangalia uwajibikaji wa mke kwa mume kama ishara ya uadilifu, anasema:

---

[2] Martina Duwe ni mwanafunzi na mtafiti wa Shahada ya Uzamivu, Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano yalifanyika tarehe 16/04/2020, mkoani Dodoma.

[3] Marryam Mwinyi ni mwanafunzi na mtafiti wa Shahada ya Uzamivu, Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano yalifanyika tarehe 07/05/2020, mkoani Dodoma.

> Kwa jamii za Kiafrika, mke kumhudumia mume katika suala la usafi wa mwili na mavazi ni wajibu. Hiki ni kiashiria cha unyenyekevu wa mke kwa mume. Mtu mwingine anaweza kuona kama ni utumwa au unyanyasaji, lakini sivyo ilivyo. Mke anatakiwa awe mtii kwa mumewe na awajibike ipasavyo. Kufanya hivyo si utumwa na si kibainishi cha kwamba mume hajiwezi, bali ni jukumu la asili pamoja na haja ya mke kudumisha mapenzi kwa mumewe.

Mawazo ya Mwinyi katika nukuu hiyo hapo juu si ya kupuuza. Swali la msingi hapa ni je, kwa nini msukumo wa kudumisha au kuimarisha mapenzi ndani ya ndoa au familia hufanywa kama ni jukumu la mwanamke zaidi ya mwanamume? Hii inadhihirisha kuwa nguvu ya mwanamke katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ni kubwa zaidi kuliko aliyonayo mwanamume.

Kazi ya fasihi inaweza kuchipuza maana nyingi kwa kuzingatia kigezo cha kiwakati na kimazingira na mtazamo binafsi wa msomaji. Jambo hili husababisha maana zinazotolewa ndani ya kazi husika kukinzana, na wakati mwingine maana hizo kukinzana na mtazamo wa kijamii. Ni katika msingi huu ambapo Martina Duwe (2020) anaweka wazi kuwa, katika kipindi hiki cha usasa, majukumu anayopewa mwanamke katika ndoa ni kibainishi cha utwezaji wa mwanamume. Hii inatokana na sababu kuwa, humweka katika nafasi ya kiumbe duni asiyejiweza. Majukumu mbalimbali ambayo alitarajiwa ayatimize au yatimizwe katika kushirikiana na mwanamke kama vile huduma za chakula, mavazi na malazi, hutegemea zifanywe na mwanamke. Wakati mwingine, kitendo cha mwanamke kumhudumia mumewe, hutazamwa kama ni kipimo au msukumo wa kudumisha mapenzi kati ya mume na mke.

**Nafasi ya kutoa maamuzi**

*Utenzi wa Mwana Kupona* ni utenzi unaomtweza mwanamume kwani unabainisha nafasi duni aliyonayo katika kutenda na kutoa maamuzi katika masuala mbalimbali. Jambo hili linabainishwa kupitia mtazamo wa Mwana Kupona ambaye anamjenga mwanamke katika daraja la juu na kuonesha kuwa maamuzi yoyote yanayotolewa na mwanamume, yawe ya kimahusiano, maisha ya ndoa au mahusiano katika jamii, yanafanywa kulingana na ushawishi unaotokana na matendo ya mwanamke. Hii inamaanisha kuwa mwelekeo wa kila jambo analolitenda au kuliamua mwanamume linapimwa katika mzani wa utashi wa mwanamke. Kwa mfano, katika utenzi huo, Mwana Kupona anamuasa binti yake kutimiza majukumu mbalimbali kwa mumewe ili ndoa yake iweze kudumu. Jukumu la mwanamke katika kudumisha ndoa ambalo linapelekea kuratibu utashi wa maamuzi yanayotolewa na mwanamume umeelezwa na Mwinyi (2020a). Anasema kuwa Mwana Kupona, kama walivyo wazazi au walezi makini katika jamii ya Pwani, alimfunza binti yake mambo muhimu kwa lengo la kudumisha mkataba au makubaliano ya ndoa.

Kimsingi, mafunzo hayo yanayohusiana na kuwa mtiifu kwa kila jambo linaloamriwa na mwanamume, kujiremba ili awe na mwonekano mzuri, kumlea kama mtoto na kumwitikia kwa kila atakalo, yalilenga kuuteka utashi wa mwanamume katika kufanya maamuzi. Kwa mfano, katika beti zifuatazo Mwana Kupona anamuusia binti yake kuwa msafi wa mwili na mazingira ili kukonga roho ya mumewe kama anavyosema katika ubeti wa 38 - 40, mtawalia:

> Na kowa na kuisinga
> na nyee zako kufunga
> na asmini kutunga
> na firashani kutia

Nawe ipambe libasi
ukae kama harusi
maguu tia kugesi
ma mikononi makoa

Na kidani cha kifungo
sitoe katika shingo
muili siwate mwengo
kwa marashi na dalia (Mulokozi, 1999:129)

Katika ubeti wa 38, Mwana Kupona anamtaka binti yake kukoga kwa kujisugua, kukosha nywele na kujipaka manukato aina ya yasmini. Katika ubeti wa 39, anamsisitizia kujipamba na kuvaa mavazi mazuri. Katika ubeti wa 40, anamsisitizia kujipaka poda yenye harufu nzuri. Kimsingi, yote haya yamekusudiwa kuziteka akili na hisia za mwanamume na kumfanya mwanamke aweze kuishi kwa amani katika ndoa yake.

Pia, katika ubeti wa 28 na 29, anamuasa binti yake kuwa mtiifu na msikivu kwa kila alisemalo mumewe kama njia ya ushawishi katika kuathiri maamuzi ayafanyayo mumewe:

Keti naye kwa adabu
usimtie ghadhabu
akinena simjibu
itahidi kunyamaa

Enda naye kwa imani
atakalo simkhini
we naye sikindaneni
ukindani huumia (Mulokozi, 1999:127)

Mwana Kupona anabainisha kuwa matendo ya mwanamke ambayo yanakitwa katika suala zima la adabu na utii kwa mume yana nafasi kubwa katika kuathiri mtazamo wa mwanamume na hivyo kufanya maamuzi kwa kuzingatia matakwa ya mwanamke. Hii inabainika pale anaposisitiza kuwa

matendo hayo ndiyo yatakayosababisha mumewe kufanya maamuzi kuhusu mkewe kama anastahili kwenda motoni au peponi siku ya kiyama. Katika ubeti wa 26 na 27, anasema:

> Siku ufufuliwayo
> nadhari ni ya mumeo
> taulizwa atakao
> ndilo takalotendewa
>
> Kipenda wende peponi
> utakwenda dalhini
> kinena wende motoni
> huna budi utatiwa (Mulokozi, 1999:127)

Kwa jumla, ijapokuwa maamuzi yanaonekana kufanywa na mwanamume, ni dhahiri kuwa utashi wa kufanyika kwa maamuzi hayo umetokana na msukumo wa matendo ya mwanamke. Jambo hili linaelezwa na Mwinyi (2020a) kuwa kitendo cha mwanamke kumtimizia mumewe kila jambo atakalo, hutweza nguvu za mwanamume na kujikuta akitekeleza wajibu katika mkataba wa ndoa kwa kumpenda mkewe katika kiwango cha juu. Ni katika upendo huu ambapo mwanamume hujikuta amefanya maamuzi mbalimbali kutokana na utashi wa mwanamke.

Kwa upande wa data za uwandani, Tatu Khamis (2020)[4] alitoa mtazamo wake kuhusu suala la maamuzi baina ya mke na mume kwa kusema:

> Mwana Kupona anaonesha wazi kuwa mwanamume ni kiumbe dhaifu na hivyo hawezi kukaa, kupanga na kuamua kwa utashi wake. Mawaidha anayompa binti yake ili kudumisha ndoa kama vile kujipamba ili awe na mvuto kwa mume, kumnyoa ndevu na mengineyo, naweza kuyatazama kama rushwa au kwa lugha

[4]Tatu Khamis ni mhadhiri na mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu kutoka Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano yalifanyika tarehe 22/05/2020 mkoani Dodoma

> nyingine ni *limbwata* linalompumbaza mwanamume huyo. Hii ina maana kwamba mwanamume huyo hana maamuzi binafsi ambayo yanasukumwa na utashi wake isipokuwa anategemea msukumo wa namna mwanamke anavyotaka iwe na iamuliwe. Kimsingi, huu ni udhalilishaji wa kiwango cha juu ambao unamfanya mwanamume aonekane kama kiumbe anayefuata upepo. Akishawishiwa kwa namna fulani, ili mradi tu ushawishi huo uziteke akili zake, basi hilo aliloshawishiwa kwalo ndilo atakalolifuata.

Hoja ya mtafitiwa huyu inapingana na baadhi ya mawazo ya watafiti mbalimbali kuwa *Utenzi wa Mwana Kupona* unamdhalilisha mwanamke. Kwa mtazamo wake, utenzi huu unamdhalilisha mwanamume kwani ametazamwa kama kiumbe duni asiyeweza kutenda jambo lolote lile kwa urazini wake, wala kufanya maamuzi ya busara isipokuwa kwa kutegemea msukumo na ushawishi kutoka kwa mwanamke.

**Thamani ya mtu na utu**

Mtazamo kuhusu thamani ya mtu na utu ni kigezo kingine ambacho kinaupima mzani wa nafasi ya mwanamke na mwanamume katika jamii. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona,* thamani ya mtu na utu wake inapimwa kwa namna mtu anavyojithamini yeye mwenyewe kimwili, yaani katika usafi wa mwili na mavazi. Katika mausia anayoyatoa kwa mwanawe, Mwana Kupona anaikweza nafasi ya mwanamke kama mtu anayethamini na kuuthamini utu wake tofauti na inavyokuwa kwa mwanamume ambaye thamani yake inawekwa katika maamuzi ya mwanamke. Kwa mfano, kumsisitizia kuhusu suala la usafi wa mavazi na mapambo kama anavyoeleza katika ubeti wa 38, 39, 40, ni kibainishi cha thamani ya mwanamke katika jamii kwa namna anavyotakiwa kuwa. Aidha, kumsisitizia mwanamke kumwangalia mumewe katika suala la usafi, kama anavyoeleza katika ubeti wa 34, ni kiashiria kuwa mwanamume ni mtu ambaye haijui thamani yake binafsi bali hutarajia kupewa au kujengewa

thamani hiyo na mwanamke. Hii inathibitika pale anapomsisitizia binti yake kuzingatia usafi wa mumewe kwa kusema:

> Mnyoe mpalilize
> sharafa umtengeneze
> na udi umfukize
> bukurata wa ashia (Mulokozi, 1999:128)

Akizingatia suala la mabadiliko ya kimazingira na hisia binafsi katika tafsiri ya kazi za fasihi, Waziri Saidi (2020)[5] aliongelea ubeti huu kwa kuihusisha thamani ya mtu katika usafi kwa kusema:

> Haya mambo hatuwezi tukalingana. Wapo wanaume wasafi wanaojithamini kimavazi na kimwili na sio lazima wafanyiwe na wanawake. Hata hivyo, inaonekana Mwana Kupona anamtazama mwanamume kama mtu asiyethamini usafi na utu wake. Suala la kumsisitiza mke kufanya usafi wake binafsi na wa mumewe, ni kiashiria kuwa kwa mwanamume usafi sio kipaumbele bali ni hisani kutoka kwa mwanamke. Kwake binafsi kuwa msafi au mchafu ni jambo la kawaida.

Kwa jumla, maelezo ya mtafitiwa huyu yanabainisha wazi kuwa *Utenzi wa Mwana Kupona* unamtweza mwanamume kwani, kupitia mausia anayopewa mwanamke, unambainisha kama kiumbe asiyeujali utu na thamani yake.

## Hitimisho

Makala hii imeonesha namna *Utenzi wa Mwana Kupona* unavyomtweza mwanamume kwa kumtazama kama kiumbe dhaifu asiyeweza kutimiza majukumu mbalimbali ya kifamilia na kijamii kwa jumla. Makala imedhihirisha hili kwa kuangalia namna Mwana Kupona anavyompa mwanamke majukumu mbalimbali, jambo ambalo linaashiria kwamba ni

[5] Waziri Said ni mwanafunzi wa shahada ya umahiri katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano yalifanyika tarehe 10/04/2020 mkoani Dodoma.

vigumu kwa mwanamume kuyatekeleza. Mwanamke kupewa majukumu hayo ni uthibitisho wa nguvu aliyonayo katika kutekeleza na kusimamia masuala mbalimbali, tofauti na mwanamume ambaye makala hii imebainisha kuwa anatazamwa kama kiumbe dhaifu. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa na kubainisha udhaifu wa mwanamume katika makala hii ni mahusiano ya kimapenzi katika ndoa, mgawanyo wa majukumu katika malezi ya familia na misingi ya kimaadili katika mahusiano ya ndoa. Masuala mengine ni nafasi katika kutenda na maamuzi katika jamii, na thamani ya utu na mtu kama inavyotazamwa baina ya mume na mke. Kwa kuzingatia tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu *Utenzi wa Mwana Kupona* kama zilivyojadiliwa na baadhi ya wataalamu waliotajwa katika makala, imethibitika kuwa kazi ya fasihi haina jibu moja. Maana zinazoibuliwa ndani yake hutegemea nadharia ya uhakiki na mtazamo binafsi wa mhakiki. Hii inatokana na mtazamo unaoibuliwa katika mjadala wa makala ambao umeiangalia nafasi ya mwanamume katika utenzi huu, kinyume na wataalamu waliotangulia ambao tafiti zao zililenga kumwangalia mwanamke anavyosawiriwa na sio mwanamume.

**Marejeleo**

El-Maawy, A. (2011). *Jawabu la Mwana Kupona. Mausiyo ya Mke wa Kisasa na Waasiya wa Mwanakupona*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Farsy, A. (1967). *Ada za Harusi katika Unguja*. Nairobi: EALB.

Gibbe, A. (1993). *Women and the Making of Literature in East Africa*. OSSREA 4th Issue Competition. Muswada.

Kezilahabi, E. (1983). "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili". *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111, Fasihi* 145 - 165.

Khatib, M. (1985). Utenzi wa Mwana Kupona. *Mulika*, 17, 46 - 52.

Mbele, J. (1985). "Women in Classical Swahili Poetry." (Muswada)

Mbele, J. (2014). "Tenzi Tatu za Kale." http://hapakwetu.blogspot.com/2014/08/tenzi-tatu-za kale.html. Imesomwa tarehe 27/04/2021

Momanyi, C. (2007). Patriarchal Symbolic Order: The Syllables of Power as Accentuatuated in Waswahili Poetry. *The Journal of Pan African Studies*, 1(8):18 - 23.

Mulokozi, M.M. (1982). Protest and Resistance in Swahili Poetry 1600 – 1885. *Kiswahili*, 49(1), 25 - 54,

Mulokozi, M.M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mwachofi, A. (1987). *Mama Eee*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mwinyi, Y.M. (2020a). Kilingo cha Utenzi wa Mwana Kupona katika Usawiri wa Mwanamke wa Pwani: Mifano kutoka Kisiwa cha Tumbatu na Lamu, (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Njozi, H. (1990). Utendi wa Mwana Kupona and Reception Aesthetics. *Kiswahili*, 57, 55 - 67.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu.* Dodoma: Central Tanganyika Press.

Sawe, A. (2018). Usawiri wa Mwanamke katika Ndoa: Mifano kutoka Utenzi wa Mwana Kupona na Utendi wa Ayubu na Matini Teule za Kidini, (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Moi.

Sengo, T.S.Y. na Kiango, S.D (1974). *Ndimi Zetu: Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longman.

Senkoro, F.E.M.K. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: DUP.

Shitemi, N. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini*. Nairobi: Kijabe Printing Press.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Senkoro, F.E.M.K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Stickney, S. E. (1840). *The Sons of the Soil.* Iliyosomwa katika http://www.indiana.edu/-letrs/vwwp/ellis/sons.html

Sturrock, J. (1979). *Structuralism and Since: From Levi Strauss to Derrida.* Oxford: Oxford University Press.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide~Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: English Press.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.